# *Mkombozi Wangu Yu Hai*

Salamu za Pasaka kwenu nyote, asubuhi ya leo. Nina furaha sana kuwa hapa, leo, maskanini, kwenye wakati huu mkuu wa ukumbusho wa Pasaka. Bwana ametupa siku njema kwa ajili ya ibada hii. Nasi tuko hapa asubuhi ya leo katika kusherehekea tukio kuu sana lililopata kutokea ulimwenguni, kufufuka kwa Bwana wetu Yesu. Yeye alikuwa mkuu katika kifo Chake, bali wanadamu wanaweza kufa, lakini hapakuwepo na mtu ambaye angeweza kufufuka katika wafu ila Yeye. Na hapo ndipo yalipo matumaini yetu asubuhi ya leo, katika kufufuka kwa Bwana wetu.

2 Nilipokuwa nikiingia, asubuhi ya leo, nikipita kwenye marefu ya kanisa, nilisimama kwa muda kidogo kule nyuma kutazama. Nikatazama huku na huku juu ya kusanyiko, ndipo nikawazia, "Watu, mapema asubuhi ya leo, wametoka nje chini ya matarajio, kutoka nje wakasikie Maneno yakisomwa, na nyimbo zikiimbwa. Na ni ukumbusho wa Yule ambaye anayashikilia maisha yetu mkononi Mwake leo hii." Niliwazia juu ya nyuso ambazo nilikuwa nikiona asubuhi na mapema, miaka mingi iliyopita. Walilala katika makaburi haya yaliyo karibu na hapa, wakingojea tukio la kufufuka kwao.

3 Nikiwazia hilo, mbona, inatuleta kwenye wazo hili, kwamba, leo tuko hapa. Hatujui ni wakati gani hasa tutapelekwa mahali pa—pale ambapo wamelala asubuhi ya leo. Na halafu basi, tukizingatia hilo, tunapaswa kuwa watu wa aina gani, na tunapaswa kuukaribia ufufuo huu wa siku ya leo namna gani?

4 Katika Kitabu cha—cha Ayubu, katika ninii wa 10... mlango wa 19 na kifungu cha 25, Maneno haya machache.

> *...Najua...mkombozi wangu yu hai,...*

5 Ulikuwa ni unabii wa Ayubu na maneno yake, akiisha kuona siku hii tunayoabudu leo hii, tunayoabudia, ufufuo.

6 Mimi, nikivuka sehemu za dunia, na kuona aina mbalimbali za dini, na namna mbalimbali za ibada, ingechukua muda mrefu, kwenda, kujaribu kueleza vioja mbalimbali vya dini za ulimwengu huu.

7 Lakini, leo hii, tukijua ya kwamba tuna siku kuu mbele yetu, na kwamba tumekusanyika hapa, asubuhi ya leo, kwa ibada hii tu ya mapema asubuhi kwa muda mfupi. Tutarudi basi makazini mwetu, kisha turudi kwa ajili ya, kile tunachoamini leo, ni ibada ya uponyaji.

8 Hatujawahi kuwa nayo ila karibu mara mbili au tatu, tangu tumekuwa—tumekuwa kwenye...katika ibada hizi. Kwa sababu, kwa kawaida, kuja maskanini na karibu na huku, watu

wetu wa nyumbani hapa, upako wa Roho Mtakatifu unaonekana kana kwamba hauji sawasawa, hapa, kwa sababu ni nyumbani. Wakati mmoja ulikuwapo, na huko chini kwenye Shule ya Upili ya Jeffersonville; na halafu ulikuwa hapa maskanini wakati mmoja.

9 Na tangu nilipoamka asubuhi ya leo. . .Inaonekana nilikuja nimechelewa kidogo, lakini hiyo ilikuwa ni kwa kusudi fulani. Nilikuwa macho asubuhi ya leo, mapema sana kabla ya mapambazuko, na kungojea.

10 Nami ninaamini tu ya kwamba tunaikabili ibada kuu leo, katika ibada ya uponyaji. Na hao wavulana, tutawapa kadi sasa, nao watazisambaza asubuhi ya leo saa tatu, kwa ajili ya huduma zijazo za uponyaji. Ninaamini Bwana atatupa wakati mzuri sana.

11 Kwa hiyo, tutamwabudu kwa maombi na katika nyimbo, na kunenwa kwa Neno, kisha nijaribu kutokuweko leo, asubuhi ya leo, saa moja, ikiwezekana, ili kila mtu aweze kurudi na kuwa na muda wa kutosha wa kujiandaa kwa ajili ya hiyo ibada.

12 Kadi za maombi zitasambazwa saa tatu kamili, kwa hiyo hazitaingiliana na ibada zingine.

13 Halafu, usiku wa leo, bila shaka, ni ibada za ubatizo, pia. Tungewataka ninyi nyote mhudhurie hii, wageni malangoni petu, na kadhalika. Tuna furaha sana kuwa nanyi asubuhi ya leo, kuona ibada hii ya mapambazuko, na maskani imejaa.

14 Sasa, juu ya mawazo tofauti sasa, leo, ya ibada ya kidini. Katika sehemu nyingi, wanaabudu mababu ambao wameaga dunia. Kwa mfano, kama tungeenda Uchina asubuhi ya leo, na kunena Neno la Mungu, ama Japani, wangeshangaa ulikuwa unazungumza juu ya mungu gani, kwa sababu, kila mtu anayekufa, ni mungu mara tu anapokufa. Na kama tukienda mahali ambapo wanaomwabudu Budha, au ninii tofauti, Waislamu, hawaamini ya kwamba Kristo alifufuka katika wafu. Hata hawaamini kwamba alikufa. Wanasema, "Alipanda farasi akaenda zake Mbinguni."

15 Lakini, leo, tuna Kweli kabisa na Nuru ya Uzima. Hakuna shaka niani mwangu, leo, kama m—mhubiri wa Injili ya Ukristo. Sina shaka hata kidogo niani mwangu, hata kivuli kimoja cha shaka, kwamba tunaamini tunayo Kweli iliyotiwa muhuri. Kwamba dini zingine huenda zikawa sawa, bali sisi tunayo ile Kweli.

16 Kama tukiangalia, leo, ya kwamba, tuangalie majira. Hakika Mungu Mkuu wa Mbinguni, aliyeziumba mbingu zote na nchi, akaumba. . .Kama unaweza kuona jinsi mawazo Yake yalivyokuwa yakifanya kazi, jinsi alivyo na majira ya kupukutika majani, mauti; kisha majira ya kuchipusha, ufufuo. Ili. . .huna budi kufa, upate kuwa na ufufuo.

17 Ni kupitia mauti ndiyo iletayo uzima kila wakati. Unaishi tu kupitia mauti. Je, uliwahi kutulia ukawazia hilo, kwamba jamii ya wanadamu huishi kupitia mauti? Kitu fulani hakina budi kufa upate kuishi; chakula. Uhai wa mimea, uhai wa wanyama, vyote hufa. Na kupitia mauti hiyo, tunakula chakula. Nacho chakula tunachokula, kitu kilichokufa cha kitu kingine, hutoa chembechembe hai za damu zinazoingia mwilini mwetu. Kwa hiyo tunaishi tu, na kukua, na kupumua, na kula, kwa uhai, na sasa. . . na kwa mauti. Basi inatubidi kuwa na mauti tupate uzima, basi.

18 Sasa, ujumbe huu tuliosomewa asubuhi ya leo, tungeuita agizo kuu, kwa maana lilikuwa ndilo agizo la mwisho Bwana wetu aliwapa wanafunzi Wake. "Kuenda ulimwenguni mwote, na kuihubiri habari hii njema, tukufu, ya ufufuo, ulimwenguni mwote, kwa ushuhuda." Na kisha angerudi. Na, kwamba, "Ishara na maajabu yangefuatana na Ujumbe huu ambao ulikuwa uhubiriwe."

19 Na leo hii, katika nchi, tunaona hata chini ya dini ya Kikristo, kwamba tunawapata watu Marekani, wengi wao, kwa heshima zote nzuri na zifaazo kwake, tunajaribu kutafuta makanisa makubwa, na makanisa makuu, na programu kubwa, na kadhalika, pia. Siku ya Pasaka, leo, makanisa makubwa na misalaba imeng'arishwa kwa ajili ya ibada hii kuu ya Pasaka. Na, leo hii, makumi ya maelfu na mamilioni ya dola yatatumika kwa maua ya Pasaka na kadhalika, kwenda madhabahuni, kuyapamba makanisa haya makubwa na makanisa makuu tuliyo nayo siku hizi.

20 Na huko Rumi, mkuu wa kanisa Katoliki, huko ndani wao. . . chumba hicho kikuu cha maiti, cha Mtakatifu Petro, ambapo watu waliokufa huzikwa. Wanapenda kusema, katika kanisa Katoliki, kwamba, "Tunayo, kwa sababu tuna mwili hapa wa Mtakatifu Petro, uliolazwa hapa. Tuna miili ya mitume mbalimbali, na wanafunzi, na ya watu wakuu ambao wamekufa na wananinii. . . Miili yao imezikwa hapa." Nao wanaitazama hiyo kana kwamba hiyo ilikuwa thibitisho kuu kwa awamu yao ya dini, ya kwamba wanaye Mungu.

21 Lakini sikuzote nimeshikilia, enyi marafiki, kwamba mambo hayo hayana maana yoyote. Sivyo. Mwanadamu yeyote anaweza kufa na kulazwa ardhini. Lakini Yule aliyefufuka kutoka humo ndiye tunayemwabudu siku hizi, Bwana Yesu aliye hai, aliyefufuka, aliyepaa juu, aliye hai leo. Watu wengi wanaweza kufa.

22 Ijumaa iliyopita, watu walitambaa kwa magoti, wakipanda vipandio vya Vatikani. Kisha watu wengi wakaingia na kusherehekea kifo, ambacho kilikuwa. . . jambo kubwa na la kuhuzunisha lililompata Kristo. Lakini ilimbidi kufanya hivyo ili kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Kristo.

23 Lakini leo ndiyo ile siku, ufufuo, huu ulikitia muhuri milele. Sasa Yeye hajafa. Yu hai, leo, anaishi katika kila moyo na kila mtu.

24 Wanaume wa kale, walipoitazamia siku hii, wale wazee wetu huko nyuma katika Biblia; Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Ayubu. Wengi wa wazee wa zamani walitazamia kwa hamu wakati ambapo Kristo angefufuka katika wafu.

25 Ninawazia juu ya Ayubu, yule tuliyekuwa tukisoma habari zake muda mfupi uliopita, aliitazamia asubuhi ya leo. Alipokuwa mzee, amezeeka, na nyama zake kwa urahisi zilikuwa zikianguka tu kutoka mwilini mwake, kutokana na vidonda. Moyo wake ulivunjika, kwa huzuni. Na kila sehemu ya mwili wake ilikuwa inanyauka.

26 Basi mtu mkuu kama huyo, ambaye aliuvutia sana ulimwengu katika siku zake; na kuona kwamba, yote aliyokuwa—aliyokuwa, na ukuu. Alisema angeenda katika miji ya Mashariki, nao watawala wangemwinamia, kwa sababu ya hekima yake.

27 Lakini huyu hapa, mwishoni mwa akili zake. Kila kitu kilikuwa kimeenda, inaonekana. Mwili wake ulikuwa umekwisha. Mali yake ilikuwa imekwisha. Watoto wake walikuwa wameangamia. Yote aliyokuwa nayo yalikuwa yamekwisha.

28 Ndipo, basi, Mungu katika rehema Zake akamshukia Ayubu, Naye akampa hisia nyingine, hata angeweza kuyafungua macho yake na kuona siku ambayo kutakuwa na mwili atakaoupokea. Alijua ya kwamba angekuja Mtu, Mwenye Haki, Ambaye angesimama mahali pake, ambaye angefufua mwili wa wafu, na angeufufua. Akasema, "Najua kwamba Mkombozi wangu yu hai." Ninapenda maneno hayo mazuri aliyolizungumzia.

29 Sio, "Natumaini hivyo. Ninajisikia atakuwako." Huo karibu ndio mtazamo wa wengi siku hizi, "Ninatumaini kwamba siku moja . . . "

30 Lakini Ayubu alikuwa na zaidi ya hayo. Alisema, "Najua Mkombozi wangu yu hai," upande wake mzuri. Sio tena katika hasi. Yote ni mazuri.

31 Na ikiwa leo hii, ikiwa tuna msalaba tu juu ya kanisa, kuonyesha (ambalo, hilo ni sawa) kwamba Kristo . . . tunaamini katika kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Kristo. Ikiwa tuna maiti chache tu za mavumbi zimelazwa chini ya kanisa, na baadhi ya watu watakatifu walizikwa mle ndani, ambapo hiyo . . . tunayo hiyo tu kama tumaini, basi sisi miongoni mwa watu wote ndio wenye mashaka zaidi.

32 Lakini, leo hii, jinsi tulivyo na shukrani! Hatuna maiti, lakini tunaye Roho aliyefufuka wa Bwana Yesu Kristo, kwamba alifufuka katika wafu, mshindi.

33 Sio tena, “Nadhani ndivyo.” Ungeweza kutazama msalaba na “kudhania ndivyo.” Ungeweza kutazama mwili uliolala chini, na kusema, “Nadhani ndivyo,” na “Natumaini ndivyo.”

34 Lakini wakati lile ono lililomgusa Ayubu limepata kuwa halisi, ufufuo wa Bwana Yesu kwa Roho Mtakatifu moyoni, basi unalo, “Najua Mkombozi wangu yu hai.”

35 Vivuli vyote vimefifia, giza lote la kale la, “kutumaini hivyo,” na “labda ndivyo,” na “tunatumamini itakuwa hivyo.” Vyote vimetoweka, kwa kila mtu ambaye amewahi kuufanya moyo wao kuwa kaburi la Bwana Yesu Kristo.

36 Akafa pamoja Naye, akazikwa pamoja Naye, na kufufuka pamoja Naye! Akafufuka pamoja na Kristo katika ufufuo! Tumaini hili jipya ambalo Mungu ameweka ndani ya mioyo yetu, siku hizi, hakikisho hili jipya! Ni matumaini kwa wale wanaoutazamia ule wakati. Lakini wakati mwanamume au mwanamke amewahi kufufuliwa upya, hiyo ni “najua hivyo” sasa. “Najua Mkombozi wangu yu hai. Kwa nini? Anaishi ndani ya moyo wangu.”

37 Si ni ajabu sana leo kwamba vivuli vyote vimepita? Yote . . . “Vema, natumaini ya kwamba nitakuja katika ufufuo.” Hakuna tena “kutumaini.” Tuna uhakika! Ni hayo tu. Tunajua hilo. Hakuna tena “natumaini hivyo.”

38 Kwa sababu, jambo fulani lilitokea maishani mwetu, ambalo liliondolea mbali vivuli vyote, wakati Kristo aliyefufuka alipokuja kwenye hali zetu za dhambi tulizokuwa ndani yake. Ndipo mambo ya kale yakafifia, katika kusulubishwa pamoja Naye, madhabahuni. Nasi tukafufuka upya, tena pamoja Naye, na kuishi pamoja Naye na kutawala pamoja Naye. “Na tumeketi sasa katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu.” Tayari tumefufuliwa pamoja Naye. Ufufuo umekwisha kupita, tuonavyo sisi, kwa sababu sasa tumefufuka pamoja na Kristo. Amina. “Tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu.”

39 Hakuna tena “kubahatisha” kuhusu hilo. Yote yamekwisha. Amina. Nalipenda tu hilo. Hakuna tena “matumaini,” hakuna tena “shauku,” hakuna tena. Loo, imekwisha.

“Sasa tumefufuka pamoja Naye, tumeketi katika mahali pa Mbinguni.”

40 Na sasa, na ndani na juu ya hili, kwa Kanisa! Unasema, basi, “Ndugu Branham, inamaanisha nini, basi, kwamba inatupasa ‘kuhubiri Injili’ yake?” Hilo ndilo tumaini letu linalofuata. Hilo ndilo jambo letu linalofuata. Baada ya kufufuka pamoja Naye, tunalo agizo kuu, kwenda ulimwenguni mwote na kuwaletea wengine habari hizi.

41 Ni asubuhi ya kupendeza jinsi gani, wakati Mariamu Magdalene, Mariamu mama yake, walipofika kaburini asubuhi

hiyo na mapema, wakishangaa, “Nani angefingirisha jiwe kutoka kaburini? Nani angeweza kuliondoa lile jiwe?” Wakaendelea mbele, mbele, kwa imani, wakiamini. Ndipo asubuhi ilipoanza kupambazuka, marobini na kadhalika wakaacha makelele yao. Ndipo jambo la kwanza, nyota ya asubuhi ikaiangaza ile njia, na kitu kama kimondo kikubwa kikasafiri duniani kote na kuning’inia juu ya kaburi alimokuwa. Ndipo Malaika akasimama pale, akalifingirisha lile jiwe.

42 Naye akafufuka kutoka kaburini, akiwa ameishinda mauti, kuzimu na kaburi. Na kusema, “Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.”

43 Na leo hii anaishi mshindi maishani mwetu, wala hakuna kubahatisha tena kulihusu. Nafikiri Pasaka ni mojawapo ya nyakati kuu sana. Kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo watu wa Injili kamili, wa kipentekoste, waliozaliwa mara ya pili, watu waliozaliwa upya, wanapaswa kuwa wakipaza sauti za sifa kwa Mungu, ni kwenye asubuhi ya Pasaka, wakati wakijua kuwa huo ni ukumbusho wa kile kilichowapata. “Wakati mmoja tulikuwa tumekufa, katika dhambi na makosa; sasa tumefufuliwa, tumeketi katika Kristo, katika mahali pa Mbinguni, tukijua Mkombozi wetu yu hai.”

44 Daudi, nabii wa kale, alisema, “Mbona, mwili wangu utakaa katika matumaini, kwa maana hatamwacha mtakatifu Wake aone uharibifu, wala hataiacha nafsi Yake katika kuzimu.” Akizungumzia juu ya ufufuo, kwamba Mungu angemfufua Kristo kulingana na Maandiko.

45 Nasi, tuliofufuliwa pamoja Naye leo, tumeketi mahali petu pamoja Naye; na sasa tayari kwa kuja kwa ule Unyakuo, tukiungojea wakati huo mkuu. “Miili yetu itakaa katika matumaini.” Tunajua hivyo. Hakuna shaka hata kidogo niani mwangu leo. Hakuna shaka hata kidogo niani mwa mtu yeyote humu, ambao wamewahi kuzaliwa mara ya pili, ila watakuwa huko kwa hakika tu kama vile kulivyo na Mbingu juu. Huna budi kuwa. Kila ahadi ni sahihi kwake. Hivyo tu. Ufufuliwe tu pamoja Naye; ndipo basi utaishi pamoja Naye, utampenda, mmeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, mkingojea wakati huo mkuu.

46 Sasa, lile agizo kuu lilikuwa, kuingia . . . Baada ya kufufuka katika wafu, ndipo Yeye . . . Lile agizo kuu lilikuwa, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Kila kiumbe kilipaswa kuisikia Injili. Hilo ndilo agizo, asubuhi ya leo, la Kanisa, ya kwamba kila kiumbe kitaisikia Injili. Ndipo, wakati kila kiumbe kitakapoisikia Injili, ndipo Yesu atarudi tena.

47 Je, uliwahi kusimama ukawazia, asubuhi ya leo, kuhusu kurudi, hiyo ni kusema, kulikuwa kumeonekana? Yeye tayari yuko hapa pamoja nasi sasa. Yeye . . . sisi siku moja . . . Sasa leo,

wazia tu kwamba Uwepo Wake uko hapa leo. Bwana Yesu yuko katika ulimwengu mwingine, ama kiwango kingine, papa hapa leo katika umbo la Roho. Roho yake inashikamana na roho yetu. Macho yetu hayawezi kumwona, kwa sababu bado ni ya kimwili, isipokuwa jambo fulani litukie ambapo tungeweza kuona ono. Lakini Yeye yuko hapa akionekana tu, halisi kama alivyokuwa siku ile alipozungumza na Mariamu, kaburini, au alipokutana na Kleopa akienda zake Emau. Uwepo Wake upo hapa.

48 Unaweza kuhisiwa na hiyo, kuhisiwa na chaji hiyo ya ndani iliyo ndani ya mwili wa mwanadamu, inayoitwa Kuzaliwa upya. Hiyo nafsi imetiwa sumaku Kwake. Na mara moja moja, ukiacha nia yako imzingatie, mkimwamini Yeye; baada ya kitambo kidogo, kitu Fulani, uhalisia, unaweza kuhisi kitu Fulani kikipitia juu ya utu wako. Hilo ndilo thibitisho la kufufuka Kwake.

Sio "nadhani hivyo." Sio "natumaini hivyo."

49 Lakini, kwa kila mtu ambaye amezaliwa mara ya pili, ni "najua hivyo." Ni, unajua. Iko pale pale, na unapowasiliana Naye. Nimewaona watakatifu wakisema, "Loo, hivi unaweza. . . " Uwepo wa Bwana u karibu. Wanasema, "Mbona, kuna kitu Fulani!" Mbona, bila shaka. Yupo pale pale. Papo hapo juu. . .Amefufuka katika wafu, na amesimama moja kwa moja karibu nawe.

50 Sasa, siku moja, tutakapoenda kuwa pamoja Naye; roho hizi humu ndani, zinazoweza kuhisi Roho huyo, zinasukuma ndani ya Huyo. Halafu basi, kwenye ule ufufuo, atakapojifanya Mwenyewe kuonekana, tutafanywa kuonekana na kuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wa utukufu. Kwa maana, tutakapokuja kutoka ulimwengu wa roho, Yeye atatuleta pamoja Naye. "Wote waliokufa katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye katika ufufuo." Loo, ni kuelimishwa jinsi gani! Ni jambo la baraka jinsi gani!

51 Loo, kama nisingechukua hili. . .Loo, kama ningaliweza kufanywa mfalme juu ya dunia nzima, na kuhakikishiwa kuishi miaka milioni moja; nisingechukua ibada ya mwaka mmoja kwa Bwana, na mambo ambayo nimeona katika mwaka uliopita, na kujifunza kwa Mungu, hata nikipewa utajiri wote wa ulimwengu. Tumaini hili lililobarikiwa! Baada ya hiyo miaka milioni moja, au chochote kile, ningekoma kuwapo.

52 Siku moja, mimi na Ndugu Cox (anayesimama nyuma ya jengo sasa) tulikuwa tumeketi kwenye ninii. . .Njia ya kuingia nyumbani, na jiwe lililovunjika lilikuwa barabarani. Mle ndani mlikuwamo na maskini mabaki ya kale ya mnyama fulani wa baharini, ama yeyote yule, aliyeishi miaka mingi, mingi sana iliyopita. Nikasema, "Angalia kitu hiki hapa."

53 Naye Ndugu Cox akasema, "Ndugu Branham, sijui huyo ana umri gani kweli?"

54 Nikasema, "Vema, Ndugu Cox, labda, wanahistoria wangesema, amefikia kwenye mamilioni ya miaka; huko nyuma kabisa kabla dunia hii haijapata kukaliwa na wanadamu, nayo maji yalikuwa yameifunika dunia. Wanyama hao labda waliishi miaka milioni nyingi, nyingi, iliyopita. Lakini mimi . . . "

55 Akasema, "Angalia, Ndugu Branham," kasema, "hivi maisha ya mwanadamu si ni mafupi sana, ukilinganisha na maisha hayo? Hebu wazia tu, hayo mabaki ya kale yangali yamesalia, baada ya mamilioni ya miaka."

56 Nikawazia, "Loo," nikasema, "Ndugu Cox, utakuja wakati ambapo mabaki hayo ya kale hayatakuwapo tena. Hakutakuwapo hata na kivuli chake. Lakini kwa sababu Yeye alifufuka katika wafu, nitaishi na wewe utaishi, milele, na kwa nyakati zisizohesabika."

57 Wakati mabaki yote ya kale yamefifia, na wakati wote wa ukongwe umepita, na vivuli vimeshuka, tutaishi, tutaendelea kuishi tena na tena, milele. Kwa sababu, kwa kukubali ufufuo wa Bwana Yesu Kristo, tunakuwa viumbe wasiopatikana na mauti, tukiugua katika Roho, tukiungojea wakati wa ukombozi wetu, kwamba sisi pia tutakuwa pamoja Naye katika Uwepo Wake uliobarikiwa, kuishi milele. Ni ajabu jinsi gani! Si ajabu iliisisimua mioyo ya watu! Si ajabu imeleta watu kuabudu.

58 Si ajabu kwamba watu siku hizi watatambaa kwa magoti yao, na kugusa mawe, na kusugua misalaba, na—na kadhalika, kwa sababu, kitu fulani ndani yao, kitu fulani ndani ya nafsi ya mwanadamu kinalilia kitu ambacho hawawezi kukipata. "Kilindi kikiita Kilindi." Na kama kuna kilindi, kinachoita, inabidi kuwe na Kilindi cha kukiitikia. Lazima kuweko tu.

59 Kwa hakika tu kama hilo jua lenye joto linavyoyaangazia mashamba, wakati yamepata uwati kutokana na baridi ya kipupwe, hapana shaka kuwepo na . . . Jua hilo limewekwa hapa kwa ajili ya jambo fulani. Chini pale, mahali fulani, pasipoonekana kwa jicho la mwanadamu, ni mimea na uhai, itakayochipuka tena kwa sababu jua lilitumwa kwa kusudi lilo hilo.

60 Na kwa hakika kama vile Nuru ya Mwana wa Mungu inavyomulika ndani ya moyo wa mwanadamu, kuna kitu kidogo mle kilichofichwa ambacho wanadamu hawawezi kukielezea. Kinaita. Hakina budi kuwepo, mahali fulani. Ninawazia hilo, nao moyo wangu unatetemeka kwa furaha, kujua ya kwamba tunao ushahidi mkuu siku hizi ya kwamba Kristo alifufuka katika wafu, sasa.

61 Nami ninawazia juu ya nyakati za Agano la Kale, pia, walipokutazamia kuja kwa Bwana Yesu, walipotangulia kumwona na kumwabudu, kwenye mawazo yake hasa. Kulikuwa na kitu ndani yao, kikiita, "kilindi kikiita Kilindi," wakingoja wakati, wakiutazamia wakati ambapo Yesu angekuja.

Sasa, leo hii, Yeye akiisha kuja . . .

62 Sasa, kule nyuma, Shetani alijaribu kuyapofusha macho ya wale waliokutazamia, kuwaambia kuwa hakukuwako na kitu kama hicho. Lakini, kwa namna fulani au nyingine, zaidi ya chochote tunachoweza kusema asubuhi ya leo, bali Roho Mtakatifu alipokuwa akiisukuma mioyo yao na kuwapa njaa na kiu, ya kwamba Mwenye Haki alikuwa yuaja.

63 Ayubu, sasa wazia, miaka elfu nne . . . Miaka elfu nne kabla ya kuja kwa Bwana Yesu, Ayubu aliuona ufufuo. Naye alipouona kwa ono, ya kwamba ungekuwako, miaka elfu nne kabla haujatukia, alikuwa na hakikisho, kwamba, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, lakini katika mwili wangu nitamwona Mungu; Ambaye nitamwona mimi mwenyewe; macho yangu yatamtazama, wala si mwingine." Kulikuwako na kilindi, kikiita Kilindi, ndani ya Ayubu.

64 Shetani anaweza kujaribu kukifutilia mbali kwa mauti. Anaweza kusema, "Naam, Ayubu, unaingia kaburini. Mabuu ya ngozi yatauchukua mwili wako." Hiyo ni kweli. Tunajua hilo.

65 Lakini Ayubu akasema, "Nitasimama katika siku za mwisho pamoja Naye." Alikuwa na hakikisho ya kwamba angekuwepo, kwa maana kulikuwa na kitu ndani ya Ayubu kilichomwambia hivyo. Na Shetani alipojaribu awezavyo kukifutilia mbali kwa mauti na kila kitu, Ayubu alilitazamia, kuliona. Alikufa katika imani, akakata roho; akafufuka tena asubuhi ya Pasaka, pamoja na Kristo, yu hai miongoni mwa wanadamu siku hizi! Haleluya! Angalieni. Si ajabu Viumbe vya Kimalaika wanaweza kuimba, "Haleluya!" Kujua!

66 Sasa, leo hii, huenda kukawa na wengine, tunaweza kusugua misalaba, tunaweza kusugua mifupa ya watu waliokufa; ni mioyo ya wanadamu ikiita kwa ajili ya kitu fulani. Wanaita. Kuna kitu fulani ndani yao, ambacho kinaonekana . . . Kwa kuwa wao ni wanadamu, wanataka . . . Wanajua kuna kitu fulani, mahali fulani, kikubwa kuliko kile wanachojua chochote juu yake, na wanakitafuta, na kukitafuta. Nao wanajaribu kukipata kwa kuabudu mifupa ya watu waliokufa, kwa kusugua misalaba, kwa kujenga makanisa makubwa.

67 Lakini, loo, kwa tumaini hilo lililobarikiwa leo, kwa hakikisho hilo lililobarikiwa, kwamba kila mtu ambaye amewahi kukutana na ufufuo, anajua, pasipo shaka lolote, kwamba Kristo amefufuka kutoka kaburini, nasi tulifufuka pamoja Naye. Tumefufuka pamoja Naye, asubuhi ya leo. Hiyo, unaona, siyo . . .

68 Ni njaa, kila mmoja wenu akimjia Kristo. Kabla hujampokea Roho Mtakatifu, ulikuwa na njaa na kiu. Ulihama. Ulitafuta. Ulisoma Biblia. Ulilia. Ulifanya kila kitu kilichoweza kufanywa.

Huenda ulikariri rozari. Huenda ulirudia shanga. Huenda ulifanya kila namna ya matendo ya kidini. Huenda uliacha kula nyama. Huenda uliadhimisha siku za sabato. Huenda ulifanya mambo haya yote ya kidini ambayo ulimwengu unazungumzia siku hizi.

69 Lakini, wakati mmoja ulipowahi kujisalimisha ukasulubiwe, ufufuo ulikuja. Huo unakupa hakikisho, la, "Najua Mkombozi wangu yu hai leo!"

> Hakikisho hilo lililobarikiwa, Yesu ni wangu!
> Loo, ni kionjo awali jinsi gani cha utukufu wa
> Kiungu!
> Mrithi wa wokovu, aliyenunuliwa na Mungu,
> Nimezawa kwa Roho Wake, nikaoshwa kwa
> Damu Yake.

70 Hiyo ndiyo habari njema. Hayo ndiyo maagizo ya jumla. Hilo ndilo agizo kuu, kwamba tunapaswa kwenda "ulimwenguni mwote, na kuihubiri Injili hii." Kuwapa watu, "katika nguvu za ufufuo." Sasa, nikitumaini kwamba . . .

71 Sasa, wakati wetu unakaribia kwisha, kwa ajili ya maskini mazungumzo haya ya asubuhi pamoja. Tunapaswa kuhubiri sasa, katika yapata saa chache, turudi tuhubiri ibada ya Pasaka leo.

72 Lakini, leo hii, katika mazungumzo haya mafupi, ni hisia nzuri jinsi gani! Ni ushirika wa ajabu jinsi gani pamoja! Nami naamini kwa moyo wangu wote ya kwamba, leo hii, maskani hii ndogo ya kale itaona ushahidi wa moja kwa moja kwamba Yesu Kristo alifufuka katika wafu, anaonekana mbele ya macho yao; Mungu akiwaponya wagonjwa, na kufanya ishara kuu na maajabu ambayo lile agizo kuu lilijumuisha. Ule upatanisho mkuu ambao ulifanywa pale Kalvari ulijumuisha mambo haya. Na, kwangu mimi, ni mathibitisho yasiyoweza kukosea ya kufufuka Kwake.

73 Akiisha kufufuka katika wafu, alisema, "Ni lazima mwende ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili hii kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

74 Nanyi mnaweza kuwa na makanisa yote makuu, na misuguo yote, na kila kitu mtakacho. Lakini nipe Nguvu za ufufuo, hata ninaweza kumwona Bwana Yesu siku hizi, kama Ua la Bondeni na Nyota ya Asubuhi. Hilo linalitia muhuri, kwangu mimi. Na kisha naweza kusema, pamoja na Ayubu wa kale, "Najua Mkombozi wangu yu hai."

> Nini kinaweza kuosha dhambi zangu?
> Hakuna chochote ila Damu yake Yesu.

75 Ni nini kinachoweza kunifanya mzima tena, kutokana na kila ugonjwa, chochote, utumwa wowote ambao niliwahi kuwa ndani yake? Si chochote ila Damu ya Yesu, na Nguvu za kufufuka

Kwake. Ni jambo la ajabu jinsi gani! Ninampenda, nanyi je? Jina Lake Takatifu lihimidiwe!

76 Sasa je, Ayubu alisikitika? Je, Ayubu aliachwa kwa sababu aliamini hili? Hasha. Hasha. Je, Ayubu alidanganywa, juu ya kile alichokiona, ufunuo wake? Je, kilindi, kikiita Kilindi, kilimdanganya Ayubu? Huenda wengi waliwazia hivyo katika siku zake. Lakini, loo, ilikuwaje mwishowe? Naye Ayubu, alipokufa, akiishakuwa mzee, Mungu alimbariki maishani.

77 Ninawaambia, angalieni watu wowote mtakao. Sikilizeni hili, enyi watu wa maskanini, nanyi wageni pamoja nasi. Maisha yoyote unayoishi, hayo ndiyo maisha unayovuna. Wewe, jinsi upandavyo, ndivyo unavyovuna. Nilikuwa na umri wa miaka arobaini na sita, hivi majuzi. Mungu amenijalia kuishi muda mrefu vya kutosha kuona kwamba huwezi kufanya makosa na kupita nayo.

78 Huna budi kufanya jambo lililo sahihi, kwa sababu Kristo amefufuka katika wafu na macho Yake yako juu ya Kanisa, Naye analitazama na kuliongoza. Kamwe usiende kinyume na hisia za Roho Mtakatifu anapokwambia ufanye jambo fulani. Haidhuru ulimwengu unasema nini, wewe fanya kile Yeye anasema ufanye. Yeye sikuzote atathibitisha Kweli na kuinyosha Kweli.

79 Sasa, wakati yeye. . .wakati nabii huyu mkuu wa Bwana, Ayubu, alipokufa na kuzikwa. Ufafanuzi mdogo tu wa yale. . .

80 Ninataka kumalizia hii ibada ndogo sasa, ili tuweze kuharakisha kwenda nyumbani, na kurudi tena kwa ibada kuu ya uponyaji. Ninaninii tu. . .

81 Mimi si mlokole. Mnajua sivyo nilivyo. Au, kama ndivyo nilivyo, sijui mimi. Lakini ninahisi tu Kitu fulani chini kabisa ndani yangu, kikisukuma na kushinikiza. Ninaamini tu ya kwamba tunakabiliwa na jambo fulani kuu, asubuhi ya leo, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Nawaambia, nisingeninii. . .Loo, jamani! Ni ninii. . .Kujua jambo hili kuu, kwamba Kristo yu hai leo hii! Ambapo, ulimwenguni kote, kila mahali, na kila dini, kila kitu kilichopo, haidhuru ni nini, kundi zima lingeikataa; hata hivyo, kwangu mimi, Yeye yu hai. Yu hai.

Ndipo basi, tutaona kama watu waliaibishwa, wanaoamini Hilo.

82 Ayubu, alipokufa, alizikwa katika sha—shamba kule. Na kaburi lake likahifadhiwa.

83 Na ndipo walipokuja manabii wa kale, Ibrahimu. Wapenzi wa Biblia, Ibrahimu na Sara. Sara alipokufa, Ibrahimu alinunua kipande cha ardhi papo hapo karibu na mahali ambapo Ayubu alizikwa, akamzika Sara. Akasema, “Mimi ni mrithi pamoja nawe huko ng’ambo.” Loo, jamani! Napenda hilo, “Warithi pamoja!”

84 Hivyo ndivyo, siku hizi, baadhi yao husema, “Vema, Ndugu Branham, unamaanisha ya kwamba ungeliacha kanisa la Baptisti? Ungefanya *hivi*, *vile*, au *vinginevyo*?”

85 Mimi ni mrithi pamoja na hawa “watakatifu wanaojifingirisha,” nami na—nataka kuwa pamoja nao. Mimi . . . Ambapo, kama Ruthu alivyosema, wa kale, “Ambako wewe . . . Watu wako ni watu wangu. Mungu wako ni Mungu wangu. Utakapokufa, nitakufa. Mahali utakapozikwa, nitazikwa.” Ninataka kufa kwa nafsi yangu, kabisa, mpaka niwe mtu mpya ndani ya Kristo Yesu.

86 Kwa hiyo, wakamzika Ayubu. Naye Ibrahimu akamzika Sara papo hapo karibu na mahali pake. Kitu fulani ndani yao; ile silika!

87 “Vema,” mnasema, “sasa, kuna jambo kama hilo, Ndugu Branham? Sasa, ulikuwa unaendelea, kuhusu dini mbalimbali. Walilisoma kutoka kwenye kitabu, pia.” Hiyo ni kweli. Walilisoma kutoka kwenye vitabu.

88 Lakini Hili si kusoma kwenye kitabu. Hili ni Kitabu kikidhihirishwa. Hili ni Neno. Ile mbegu ikaanza kukua, yaani, “Najua.” Kama unasoma tu barua, utasema, “Natumaini hivyo. Ninaamini hivyo.” Lakini wakati mbegu inapofanywa Hai, basi unajua hivyo. Amina. Amina. Loo, ni “kujua hivyo.”

89 Ayubu alisema, “Najua!” “Nililitumainia; nililiamini; nimetoa dhabihu; nimefanya mambo haya yote; nilitumaini hivyo.” Lakini lile ono lilipokuja, naye akaliona, alisema, “Ninajua.” Jambo fulani limetokea.

90 Unaweza kwenda kanisani. Unaweza kukariri Kanuni zote za Imani ya Mitume. Nawe unaweza kufanya mambo haya mengine yote ambayo ni ya kidini. Unaweza kubatizwa kwa namna yoyote unayotaka kubatizwa. Unaweza kufanya lolote la mambo haya unayotaka. Lakini mpaka nafsi yako imeamshwa na ufufuo wa Bwana Yesu, wewe . . . “Matumaini” yote yametoweka basi, na “kujua hivyo” kumeshuka. “Najua!”

Ayubu alisema, “Najua Mkombozi wangu yu hai.”

91 Ibrahimu alisema, “Nimekuwa na ono la aina ile ile. Wakati kule juu mlimani, wakati (Kristo) Mungu alipokutana nami, na kunipa . . . majina Yake ya ukombozi, kama Yehova-yire, Yehova-rafa, na hayo yote; nikiona kifo, kuzikwa, na kufufuka. Nilipoiona, na nikaitoa ndani ya mwanangu mwenyewe, nilipomwona mtoto Isaka (Mama ya huyu mama aliyekufa hapa, mvulana wake.), nilipompeleka mlimani, nikamwacha abebe kuni zake mwenyewe, kwenye kilele cha mlima,” Mwanzo 22, “na hapo yeye . . . Nikamlaza juu ya madhabahu nami nilitaka kuutoa uhai wake mwenyewe. Nikijua kwamba nilikuwa nimempokea kama mtu kutoka kwa wafu, niliamini kwamba Yeye angemfufua tena. Na kupitia tumaini hili kuu linalopiga moyoni mwangu, najua Yeye alisema ya kwamba angeweza

kumfufua." Mnaona? Ilikuwa ni utangulizi wa ule ufufuo; kitu kile kile alichokuwa nacho Ayubu.

92 Hivyo akasema, "Sasa, mimi ni mrithi pamoja na Ayubu, kwa hiyo nizikeni katika uwanja ule ule." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo wakampeleka kule, wakamchukua Sara na kumzika karibu na Ayubu. Ibrahimu akasema, "Sasa kwa kuwa wao . . . Shamba hili linaweza kuuziwa mtu mwingine, au kwa maana wewe ulinipa. Sitaki unipe. Nataka kulilipia. Ingawa unanipa, nataka kulilipia."

93 Na hivyo ndivyo, kila mtu, hiyo ni, "Kwa neema mmeokolewa, sio kwa matendo," hakuna unachoweza kufanya. Lakini kama ukiwahi kupata ufufuo uliobarikiwa moyoni mwako, ukitaka kuishi maisha ya Mkristo, shauku ya moyo wote ndani yako ni kufanya yaliyo mema. Loo, ninalipenda tu! Sio kwamba unalazimika kufanya *hivi*. Sio kwamba ni wajibu kwako, lakini kuna kitu Fulani ndani yako kinachokufanya utake kulifanya. Unataka kulifanya. Hulifanyi kwa sababu ni wajibu. Unalifanya kwa sababu ya upendo.

94 Unasema, "Najua. Vema, sina budi kuamka na kuwatayarisha watoto kwenda kanisani asubuhi ya leo. Loo, jamani!" Unaona? Loo, jamani! Hujagusa ufufuo.

95 Ndugu, ufufuo unapoingia moyoni mwako, unatamani kulifanya. Kuna kitu, ambacho huwezi kujiepusha nacho; Kitu humo ndani.

96 Ayubu, alipoona jambo hili! Naye Ibrahimu akaliona; alimzika Sara karibu na Ayubu. Akalinunua hilo shamba, akalinunua kwa pesa zake, ili liwe na uhakika. Akaweka mashahidi mbele yake, kwamba alihakikishiwa kwamba alinunua shamba hili liwe mahali pa kuzikia. Na halafu, Ibrahimu mwenyewe, alipokufa, alizikwa pamoja nao, pia, katika shamba lile lile.

97 Ibrahimu akamzaa Isaka. Ndipo Isaka alipokufa, alizikwa pamoja na Ibrahimu; chini ya ono lile lile, wazo lile lile, "kilindi kile kile kikiita Kilindi," kile kile "Najua Mkombozi wangu yu hai." Jambo lile lile, ushahidi ule ule.

98 Halafu basi Isaka akamzaa Yakobo. Naye Yakobo akafa, huko chini kabisa Misri, mbali sana na nchi hii.

99 Naye alikuwa mlemavu. Alitembea tofauti na alivyokuwa akitembea, kwa sababu usiku mmoja alikutana na Malaika wa Mungu. Naye Bwana akaigusa nyonga yake na kumfanya atembee tofauti. Alikuwa na thibitisho ya kwamba alikuwa ameshikwa na Mungu, naye Mungu alikuwa amemshikilia. Na hivyo ndivyo, alipopata ushahidi huo, maskini nyonga hiyo iliyolemaa aliyokuwa akitembelea pale, na kumfanya atembee sawa.

100 Upande mmoja, mtu anayejisifu sana, nanii mkuu. . . Vema, kile alichoitwa kweli, alikuwa mdanganyifu. Aliitwa "mdanganyifu." Neno lenyewe *Yakobo* linamaanisha "mdanganyifu." Naye alipokuwa upande huu, mdanganyifu; mdanganyifu mkubwa, mwenye nguvu, mwenye afya.

101 Upande ule mwingine, mfalme anayechechemea aliyekuwa pamoja na Mungu; akaguswa, tofauti, alikuwa na tumaini hilo lenye baraka ndani yake! Alitembea tofauti. Alitenda tofauti. Aliishi tofauti.

102 Ndipo alipokuwa anajitayarisha kufa, huko mbali sana Misri. Liwazie hilo sasa. Pamoja na uvuvio huo kabla ya ule ufufuo, aliopewa kwa kipimo, kabla ya ule ufufuo. Akasema, "Ninajua jambo fulani litakalotukia kule Misri, moja. . .si katika Misri; bali huko juu katika nchi ya ahadi, moja ya siku hizi. Kwa hiyo juu ya mahali pale pale ambapo uvuvio huu. . . Njoo hapa, mvulana wangu, Yusufu," ambaye alikuwa ni nabii. Akasema, "Njoo hapa na uweke mkono wako hapa, 'kushindana mwereka,' mahali ambapo nimekuwa. Na uniapie, kwa Mungu wa Mbinguni, ya kwamba hutanizika hapa chini. Apa kwamba hutanizika hapa." Kwa maana, alijua ilikuwa muhimu kwamba akusanywe pamoja na hao watu.

103 Hiyo ndiyo sababu, siku hizi, tunataka kuimba tunapoweka mikono yetu juu ya msalaba wa kale unaoparuza, "Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa; ingawa itashutumiwa, ingawa itadhihakiwa, ingawa ninaweza kuwa mtu mashuhuri, maarufu hapa."

104 Vivyo hivyo, siku moja, tuseme, maskini mvulana mdogo alitembea kote mjini hapa, na kidogo ni maarufu kati ya. . . kadhalika, wale jamaa wadogo. Lakini niliona kitu fulani siku moja, kilichoingia humu ndani. Nami nikachukua upande wa kuchechemea, upande huo mwingine.

105 Je, huna furaha, asubuhi ya leo, ulichukua mahali pako kule? Kwa maana kulikuwa na kitu fulani ndani—ndani yako!

106 Msichana mmoja, nilipokuwa tu mhubiri mvulana, hapa mahali nilipokuwa nikihubiri, yeye, nilimpeleka kanisani usiku mmoja, akasema, "Billy, tutaninii. . . baada ya kanisa, tunaweza kwenda kwenye sinema?"

Nikasema, "Siendi kwenye sinema."

107 Akasema, "Vema," kasema, "tungeweza—tungeweza kufanya a—ahadi ya kuonana, au miadi, kwenda kwenye dansi iliyokuwa inaenda kuwako?" Naye huyo msichana alikuwa mwalimu wa shule ya Jumapili.

108 Nami nikasema, "Mbona, la." Ndugu yake alikuwa mhudumu. Yeye haishi mbali sana na papa hapa. Naye. . . Kasema, "Je, tunaweza kwenda kucheza da—da—dansi?"

Nikasema, "Sichezi dansi."

109 Naye akasema, “Ati huchezi dansi?” Kasema, “Kwani unapata raha yoyote wapi jamani?”

Nikasema, “Shuka uje kanisani, nitakuonyesha.” Amina.

110 Nitakwambia, ndugu, ninapohisi ule ufufuo, nguvu za kugeuza za Bwana Yesu Kristo ukizunguka kupitia mwili wa mwanadamu, ambao unatoa hakikisho hilo kamilifu, kuna furaha zaidi katika Huo, katika dakika tano, kuliko ilivyo katika anasa zote za dunia ambazo zingeweza kutolewa. Hizo Nguvu za kufufuka!

111 Vema, usiku huo wenye dhambi walikuja madhabahuni. Alikuwa ameketi kule nyuma akilia, pia. Nikasema, “Sasa, angalia, dada, unaona furaha yangu ilipo?” Nikasema, “Nina furaha zaidi sasa hivi kuliko vitu vyote unavyoweza kutoa ulimwenguni. Ulimwengu, na nguvu zake zote, usingeweza kamwe kuchukua mahali pa Hili.” Kuwaona watu wakija, kuna kitu Fulani mle ndani!

Kusema, “Naam, ni nini? Hiyo si kazi yako.”

112 Loo, naam, ni kazi yangu, pia. Ni kazi ya kila mwanamume na mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, kuona Wakristo wakiingia katika Ufalme wa Mungu. Ni wajibu wako. Ni kazi yako. Na ni furaha jinsi gani wakati yote yanapotokea, tena, unaona ni amani ya jinsi gani. Naam.

113 Yakobo akasema, “Sasa weka mkono wako hapa, na kuapa kwamba hutanizika hapa.” Kwa hiyo wakamchukua na kumzika huko juu pamoja na hao wengine.

114 Halafu basi—basi, Yusufu, kwa namna fulani ilitoka kwa Yakobo ikaingia kwa Yusufu. Ndipo wakati Yusufu alipokufa kule Misri, alisema, “Sasa, angalieni, msinizike hapa kwa sababu ninajua siku moja tutaondoka huku. Kwa hiyo, mimi . . . Muiache tu mifupa yangu nje ya ardhi.” Loo, jamani! “Ninataka kutoa kila ushuhuda niwezao, ninaliamini.” Hiyo ni kweli. Kasema, “Nikiisha kufa, iacheni tu mifupa yangu pale kwa ajili ya ushuhuda.” Mnaona? Ni nini? Angeweza kusema mengi kama Ayubu, “Najua Mkombozi wangu yu hai,” maana alikuwa ameona jambo lote likiigizwa. Alikuwa ameona, kama Ayubu.

115 Ayubu aliliona katika ono. Ibrahimu aliliona kwa Isaka. Naye Isaka ambaye. . .na Yakobo, na kadhalika. Na Yakobo aliona kwa kushindana mwereka.

116 Sasa Yusufu aliliona kwa maisha yake mwenyewe. Aliona ya kwamba alizaliwa mvulana wa kipekee, ya kwamba alikuwa mwonaji. Kulikuwa na kitu fulani kumhusu; aliweza kuona maono. Hakuweza kuelewa. Hata akaenda na kuona . . . Aliwaambia mama na baba yake, walipojaribu kumsahihisha, alipoona miganda yote ikimwinamia. Hakuweza kuelewa. Lakini basi, jambo lililofuata, aligundua kwamba alisalitiwa na

ndugu zake. Akasema, "Ninaonyesha nini hapa? Ni ujuzi gani huu wa awali ninaopokea?" Aliangalia maisha yake mwenyewe.

117 Na mtu yeyote anaweza kutazama maisha yako mwenyewe na karibu kujua jinsi ulivyo, ikiwa tu utajichunguza mwenyewe, kama wewe ni Mkristo kweli au la. Angalia mambo unayofanya, na yale unayosema, na unaoshirikiana nao, na kadhalika. Utagundua kama kweli una chochote hapo, au huna.

118 Aliyaona maisha yake yalipoanza kusogea. Ndipo muda si muda mwajua, waliona ya kwamba alitupwa shimoni; akadanganywa na ndugu zake, akidhani ya kwamba aliuawa na kutupwa shimoni, na kutolewa tena. Yusufu aliliona hilo. Alijiona gerezani. Alijiona yuko shimoni. Aliona Mungu alikuwa pamoja naye, lolote alilofanya, wajua, yeye alikuwa mfalme wa mafanikio. Ulimwengu ulifanikiwa. Kila mahali Yusufu alipokuwa, palikuwa na mafanikio, kwa kuwa alikuwa mfalme wa mafanikio. Naye, yeye, akimfananisha Kristo kimbele.

119 Popote alipo Kristo, kuna mafanikio. Naye Kristo atakaporudi duniani, laana yote ya duniani itaondolewa, baadhi ya siku hizi. Maskini jangwa litachanua kama waridi, na mahali panapoparuza patanyoshwa. Nayo itazaa kwa wingi, kwa maana Yeye ndiye Mfalme wa mafanikio, popote alipo. Haleluya! Mfalme wa mafanikio!

120 Jinsi tungeweza kukaa juu ya hili kwa yapata saa moja hivi sasa! Lakini, ili kuharakisha sasa, inatubidi kuharakisha.

121 Sasa mwangalie Yusufu, akiliona wakati huo, wakati alipojua kila kitu alichofanya. Aliwaona ndugu zake waliomsaliti, hatimaye wakimjia, bila kujua yeye alikuwa ni nani; na kusujudu mbele zake, kwa kicho. Nao wale waliomsulubisha, tuseme, waliomtupa ardhini, wale waliomwuza kwa Wamisri, wote waliomdhulumu, walisimama mbele zake. Na, yeye, mtawala mkuu; wakatetemeka. Nao wakasema, "Loo, hilo . . . " Wakatetemeka, kwa sababu, walisema, "Tumemwua ndugu yetu." Na yote kuhusu hilo, na jinsi ambavyo ilipaswa kuwa katika kivuli.

122 Yusufu, alijua ya kwamba hizo zingekuwa ndizo hali za ulimwengu wakati wa kuja kwa Bwana Yesu, kwa hivyo akaitaja mifupa yake. Akasema, "Msinizike hapa. Bali nataka kuacha kila ushuhuda niwezao, ya kwamba ninaamini ya kwamba siku moja kutakuwako na ufufuo, huko ng'ambo, ambako wale ambao wamekuwa na uvuvio uo huo wametangulia."

123 Na ndivyo Kanisa lingeweza kusema, asubuhi ya leo! Ingawa "kwa ulokole," kama tunavyoitwa; ingawa kwa sababu tunaamini katika Nguvu za ufufuo; ingawa tunaamini katika uponyaji wa Kiungu na ishara zote za kimbinguni ambazo Kristo aliahidi; inatulazimu kuchukua upande wa "wasiojua kusoma na kuandika," au "walokole," na kadhalika! Haileti tofauti yoyote yale yanayotulazimu kuchukua, mradi tu tunajua

Mkombozi wetu yu hai, naye ameleta ushahidi moyoni mwetu, kwamba yu hai na anatawala.

124 Yusufu akasema, "Ninataka kutoa kila ushuhuda dhidi ya ibilisi ninaoweza."

125 Kwa hiyo akaitupa mifupa yake kule nje, nayo ikakaa kule kwa muda wa miaka mia nne. Amina. Kwa maana, ilitazama kupita hapo! Watu wanasema, "Ni mlokole jinsi gani!" Ilionekana kana kwamba, basi, mlokole, bali ikathibitika kuwa ni Kweli. Amina.

126 Ndivyo itakavyokuwa kwa kila mtu aliye na tumaini hili lenye baraka la somo hili asubuhi ya leo, "Najua Mkombozi wangu yu hai. Najua, haijalishi ni nini!"

127 Wanasema, "Loo, tunafanikiwa hapa. Misri yote imefanikiwa wakati tukiwa hapa," mambo haya yote.

128 Lakini hilo halikuleta tofauti yoyote. Alijua watatoka kule, bila shaka kabisa. Akasema, "Sasa, ichukueni mifupa yangu kule juu, mkaizike huko Misri. . .huko juu katika nchi ya ahadi, huko katika nchi ya Kanaani, nje ya Misri." Kwa hiyo wakati wao. . .Musa aliingia, nabii mwingine aliyevuviwa, naye akaitwaa mifupa ya Yusufu, akaichukua, na kuizika katika shamba lile lile, mahali pale walipozikwa hao wengine. Alishika njia yake, pamoja na hao wengine. Kwa nini? Kulikuwa na kitu Fulani ndani yake. Kitu ndani yake! Haidhuru. . .

129 Huwasikii watu hao wengine kule chini wakisema lolote kulihusu. "Vema, mahali popote ni sawa." Wanaanguka tu popote watakapo.

130 Lakini kulikuwa na kitu Fulani ndani yake, kitu Fulani kilichokuwa na ono lile lile ambalo Ayubu alikuwa nalo, ono lile lile hao wengine walilokuwa nalo. Haidhuru walimwengu wengine waliwazia nini, walichofanya, hilo halikuwa na uhusiano wowote na Yusufu; hilo halikuwa na uhusiano wowote na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, na hao wengine wote. Kitu fulani kiliwasukumia kwenye nchi hiyo ya ahadi. Ilionekana kuwa ni ulokole, lakini waliitaka kwa sababu kulikuwa na kitu Fulani ndani yao. "Kilindi kikiita Kilindi."

131 Ndivyo ilivyo leo hii kwa kila mwaminio. Kuna kitu Fulani ndani yao, ambacho kinasukuma kwa Hilo. Haidhuru, unaweza kujaribu *hili, lile,* ama *linginelo,* lakini kuna Kitu Fulani kinachosukuma. Unajua, bila shaka lolote, ya kwamba kuna Mji ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga ni Mungu. Unajua ya kwamba kuna kitu Fulani kule, kwa hiyo wewe jisukumize Kwake.

132 Sasa, siku walipomzika, ile mifupa kule juu, mamia ya miaka yakapita.

133 Ndipo hatimaye, siku moja, "Kwa ajili yetu Mwana alizaliwa, tulipewa Mtoto. Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri,

wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Mfalme wa Amani, Baba wa milele." Naye akaja duniani, Naye akaja kwa njia ya hori, masikini na duni.

134 Lakini kitu Fulani ndani Yake, ambacho kilijua! Alisimama pale akiwa na unabii mmoja kutoka katika Biblia. Akasema, "Uharibuni mwili huu, na katika siku tatu nitaufufua tena."

135 Alikuwa ndiye Mtu pekee ambaye angeweza kusema hivyo, aliyewahi kutoa hilo tamshi, ama atakayeweza kulitoa. "Ninao uwezo wa kuulaza mwili Wangu chini; ninao uwezo wa kuutwaa tena." Hiyo ni kweli, Imanueli, Mwenyewe!

136 Halafu basi alipokufa, na, siku ya kufa Kwake, wakamshusha kutoka msalabani, wakamlaza kaburini. Naye akalala mle tangu Ijumaa alasiri hadi Jumapili asubuhi, kwenye asubuhi hiyo ya ajabu ya Pasaka alipofufuka tena. Nayo nafsi Yake ikafunguliwa kutoka katika magereza ya kuzimu kule chini, ambako aliendа kama mwenye dhambi kwa ajili yangu na yako, akizichukua dhambi zetu, ili kutupa hakikisho kamili. Hakuna sababu ya kutilia shaka, tena; lipe hakikisho kamili. Alisema, "Mimi . . ."

137 Kwa sababu Yeye alifanya hivyo, nafsi Yake ilitupwa kuzimuni, kwa sababu Yeye alikuwa mtu aliyetupwa. Alikuwa ndiye yule "mbuzi wa Azazeli" wa Agano la Kale, ambaye, waliweka dhambi za watu juu ya yule mbuzi wa Azazeli na kumwelekeza nyikani apate kufa. Yesu alikuwa yule mbuzi wa Azazeli aliyejitwika dhambi za watu, naye akatupwa na kwenda kuzimuni, apate mateso. Mwili wake ukaingia kaburini, kulipia gharama ya ufufuo wetu. Loo, jamani!

138 Ndipo, katika asubuhi hiyo ya Pasaka, aliporudi kutoka kaburini, ambako maumivu ya mauti na kuzimu hayangeweza kumshika. Ndipo wakati alipofufuka tena kwenye asubuhi ya Pasaka, si kwamba tu Yeye alifufuka, bali vivyo hivyo walitokea Ayubu, Yakobo, Ibrahimu, Isaka. Hao wengine wote wakaja katika ufufuo, katika Mathayo 27, "Na kuonekana na wengi, na kote mitaani." Huo ulikuwa ndio muhuri wa ushuhuda wao, kwa sababu walikuwa na kitu fulani ndani yao, kilichosema, "Najua Mkombozi wangu yu hai." Na kwa kila mtu . . . Sasa, walijua!

139 Mungu alijua, ya kwamba katika siku zijazo, ya kwamba wanatheolojia wangeishika Biblia hii. Walijua ya kwamba watu werevu wangeishika, kwamba wangeweka tafsiri yao wenyewe Kwake, kwamba wangesema, "Loo, haimaanishi *hivi*. Haimaanishi *hivyo*."

140 Kwa hiyo, ili kuhakikisha, kwamba mipango Yake mikuu katika nyakati zijazo itatimizwa . . . Sikilizeni kwa makini sasa tunapofunga ibada. Kama katika nyakati zijazo, kwamba mpango Wake utatimizwa, Mungu alitoa shahidi wa hakika kwake.

141 Tunaweza kulisoma na kusema, "Ninaliamini." Hiyo ni kiakili. Hiyo ni imani ya kiakili. Hiyo ni theolojia ya kiakili. Lakini kuna kitu Fulani zaidi ya hicho. Hiyo ni kweli.

142 Sio kwamba tu alifufuka kutoka kaburini, bali alipaa Juu na kumrudisha Roho Mtakatifu. "Alipaa juu, akawapa wanadamu vipawa; aliteka mateka, na kuwapa wanadamu vipawa."

143 Na, siku hizi, baada ya wanatheolojia kuichezea Biblia, baada ya madhehebu ya kanisa kuundwa, nao wanasema, "Naam, *hii* ndiyo tunayohitaji. Watu wengine wamezikwa chini ya kanisa, baadhi ya watakatifu; tutaichimbua mifupa yao na kuileta hapa." Baadhi yao walisema, "Tutajenga kanisa juu ya kaburi ambapo Yeye—ambapo Yeye alisulubiwa, au mahali alipozikwa. Tutajenga kanisa hapo." Watu, katika nyenzo, wanajaribu kufanya mambo ya kimwili, lakini ni bure kabisa. Hakuna kitu kwake. Yote ni upuuzi, wala hakuna chochote kwake.

144 Lakini ufufuo wa kweli ni wale waliokufa pamoja Naye, wamezaliwa mara ya pili, ambao wana hiyo imani ya "kujua hivyo." "Najua Mkombozi wangu yu hai." Naye Mungu anafanya kazi na watu hao, "kwa ishara na maajabu," na lile agizo kubwa hapa, akionyesha kwamba alifufuka katika wafu, na kuonyesha ishara na maajabu yanayoonekana.

145 Mungu awabariki. Je, mnaamini hivyo? Je, unaamini kwa moyo wako wote?

146 Naomba tuharakishe twende nyumbani sasa. Mkale kifungua kinywa chenu na kurudi tena saa tatu. Nasi tutawatuma hao wavulana huko nje, wakasambaze kadi za maombi, saa tatu.

147 Na kwangu . . . aisee, asubuhi ya leo, na maneno ya mwisho juu ya hili hapa, mpaka nitakaporudi. Bwana Yesu yeye yule aliyefufuka katika wafu yu hai leo, na anaweza kufanya mambo yale yale kama alivyoahidi. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, hata nitakaporudi tena." Ingawa umetupwa nje, ingawa unaitwa "mlokole," hata hivyo Yeye yuko hapa katika Nguvu Zake zote. Mungu awabariki. Ninaomba kwamba Mungu atawapa Pasaka, leo, ambayo hamtaisahau maadamu mko hai.

148 Sasa, mnasema, "Je, unawapinga, hao watu wanaoenda makanisani, na misalaba mikubwa, na kadhalika?" La, bwana, ndugu yangu. Mambo hayo, kadiri yanavyoweza kuwa mazuri, ni kama tu kupata . . . Hivi ndivyo ninavyofikiria kuhusu makanisa hayo makubwa.

149 Unasema, "Loo, hakika, kama Bwana angetupa mahali pakubwa mno, ningefurahia."

150 Lakini huu hapa uchanganuzi wangu wa jambo hilo. Uliwahi kufikiria kwenda hapa chini pa kuyeyushia chuma kuvipa maumbo na viwanda, na wakijenga gari-moshi kubwa, refu la

abiria, maridadi, na viti vya kupendeza sana, vilivyong'arishwa, na filimbi kubwa juu yake, na kuweka wahandisi mle ndani, bila mvuke wowote wa kuivuta? Unaona? Unaninii tu. . . Haingefaa kitu hata kidogo. Ni afadhali niwe na gari la mkono mahali fulani, lenye mvuke ndani yake, kuliko kuwa na hayo yote, (nawe je?), kwa sababu utaenda mahali fulani. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo sasa kwa urahisi kumbukeni tu huo, ule ufufuo wa kweli, kitu halisi.

151 Unasema, "Kitu hicho kinaweza kujiendesha chenyewe, huko nje." Kinawezaje kwenda? Nithibitishie.

152 Na hivyo ndivyo tumefanya. Tumevirembesha viti. Tumepiga filimbi msasa. Tumewasafisha wanachuoni hodari, wakafundishe theolojia kuu, na kutumia maneno makubwa mno ambayo yataninii tu. . . mambo makuu ambapo karibu wanajifunza kamusi, usiku kucha, kwa ajili ya mahubiri, wapate kuyahubiri kesho yake asubuhi, "kwa maneno makuu mno." Lakini, ndugu, kwangu mimi, huo ni upuuzi.

153 Nipe Kristo. Nipe ufufuo. Nipe ushahidi, moyoni mwangu, kwamba Kristo alifufuka katika wafu. Hilo latosha, kwangu mimi. Amina.

154 Nipe kitu ninachoweza kusema, pamoja na Paulo wa kale, kwenye kile chumba kikubwa, chenye giza kilichowekwa pale mbele yangu, kama mwanadamu. Wala mimi sio mtoto tena, kwamba najua kila wakati moyo wangu unapopiga, ninaelekea kwenye kile chumba kikubwa cha giza kinachoitwa mauti. Kila wakati; na siku moja itachukua pigo lake la mwisho, nami sina budi kuingia katika chumba hicho cha mauti pamoja na kila mwanadamu.

155 Lakini nataka kusema, pamoja na Paulo mtume huyo mkuu, kama alivyosema. "Nataka kumjua katika Nguvu za kufufuka Kwake," hata, atakapoita kutoka miongoni mwa wafu, nitatoka pamoja Naye wakati huo. Hivyo ndivyo ninavyotaka, "kumjua Yeye," asubuhi hii. Hivyo ndivyo, namshukuru Mungu, "Ninamjua katika Nguvu za kufufuka Kwake." Kwamba, "Najua Mkombozi wangu yu hai."

156 Macho haya yaliyopofushwa, ambayo wakati mmoja yalikuwa mapofu, yamefunguliwa. Maskini mwili huu mdogo, ulio dhaifu, wa kama pauni mia moja na ishirini na tano, unaoyumbayumba hapa, umekuwa. . . nyama imekuja juu yake. Moyo huu ambao wakati mmoja ulikuwa mweusi kwa dhambi umefanywa kuwa mweupe. Tamaa hizi zilizokuwa zinayapenda mambo ya ulimwengu, zimekufa, miaka ishirini na miwili iliyopita, na zimefufuka tena sasa.

157 Na macho haya ya kibinadamu ninayoangalilia, nimejaliwa, kwa neema ya Mungu, kuona viwete wakitembea, vipofu wakiona, loo, ishara kuu na maajabu, na nguvu za Mungu. Najua Mkombozi wangu yu hai. Ninajua hilo, bila shaka

lolote. Ninajua. Ninajua. Ninajua. Mkombozi wangu yu hai, amina, daima, wakati wote. Hata nguvu zangu zikiisha ndani yangu, hata ulimi wangu ukishikamana na midomo yangu, hata mabuu ya ngozi yakiula huu mwili, hata jiwe la kaburini likisimamishwa, hata hivyo, najua Mkombozi wangu yu hai. Amina.

Na tuombe.

158 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa ajili ya ufufuo huu. Ee Mungu! Wakati mmoja, mwenye dhambi, aliyefungwa minyororo ya dhambi; wakati mmoja gerezani, pamoja na hali za mambo; ya usumbufu, ya mizuka, akiogopa mauti, akiogopa kukutana Nawe, lakini siku moja tukufu kulikuja ufufuo kutoka kwake. Kristo alifufuka moyoni, na leo hii tuna hakikisho hili kuu. Leo hii Yeye anaishi kwa uweza mkuu kabisa, nasi tunakushukuru kwa ajili Yake.

159 Nasi tunaomba, Baba, sasa, ya kwamba utabariki kusanyiko hili dogo, nasi tumekusanyika. Roho Wako Mtakatifu na atulie juu ya kila mmoja. Uwe pamoja nasi katika ibada ijayo, Bwana. Na naomba Roho Mtakatifu aje katikati yetu asubuhi ya leo na kumponya kila mgonjwa aliyeko jengoni. Tujalie, Bwana. Jalia watu waondoke hapa, waikumbuke Pasaka hii milele. Tujalie, Bwana. Na jalia mamlaka kuu, naomba Malaika wakuu, waliolifingirisha lile jiwe kwenye asubuhi ya Pasaka, na wasimame sasa hivi, leo hii, kufingirisha na kuondolea mbali kila jiwe la shaka, kila woga, kila mafarakano. Liondoe kutoka mioyoni mwa watu. Tujalie, Bwana, kwamba Roho Mtakatifu aweze kushuka katika nguvu kuu, na kuweza kumfikia kila mmoja. Tujalie. Kupitia kwa Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

160 Hebu tusimame.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa Roho Mtakatifu,
Alikuwa Yohana Mbatizaji, lakini alikufa kama mwanamume;
Ndipo akaja Bwana Yesu, walimsulubisha,
Alihubiri kwamba Roho atamwokoa mwanadamu kutoka kwa dhambi.

Inaendelea kudondoka damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Loo, ndipo wakampiga kwa mawe Stefano, alihubiri dhidi ya dhambi,
Iliwakasirisha sana, wakakiponda-ponda kichwa chake;

Lakini alikufa katika Roho, akakata roho,
Na akaenda kuungana na wale wengine, jeshi hili linalotoa uzima.

Kulikuweko na Petro na Paulo, na Yohana mtakatifu,
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate kuangaza;
Waliichanganya Damu yao, kama wale manabii wa kale,
Kusudi Neno la kweli la Mungu lipate kuhubiriwa kwa uaminifu.

Kuna nafsi chini ya madhabahu, zinalia, "Hata lini?"
Bwana apate kuwaadhibu wale waliotenda maovu;
Lakini kutakuweko na wengine watakaotoa damu ya uhai wao,
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na mafuriko Yake mekundu sana.

Inaendelea kudondoka damu . . .
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

161 Hivi hamumpendi? Tunaimba wimbo huo mdogo kwa sababu tunaamini ya kwamba Injili ya Roho Mtakatifu ingali inadondoka Damu. Ni njia ya mateso. Ni njia ya kutokuelewana. Hiyo ni sawa. Ulimwengu hauijui. Ulimwengu haukuijua kamwe. "Ulimwengu utawachukia. Lakini jipeni moyo, Mimi nimeushinda ulimwengu." Hawaelewi Hilo. "Mahubiri ya msalaba ni upumbavu kwao wanaopotea." Lakini kuna kitu Fulani chini katika moyo wa mwaminio, kinachosema, "Najua Mkombozi wangu yu hai. Najua, bila shaka."

162 Kila mtu anajisikia vizuri? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa peana mikono na mtu anayesimama karibu nawe, useme, "Bwana asifiwe." Bwana asifiwe. Bwana asifiwe. Bwana asifiwe. Hilo ni sawa. Hilo ni sawa.

163 Chukua mahali pako, asubuhi ya leo, pamoja na Kristo. Alifufuka katika wafu. Shika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Vema.

Sasa na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo.

164 Na sasa kumbukeni zile ibada katika dakika chache tena. Tunaanza tena, sasa, saa—saa tatu; kadi za maombi zitasambazwa. Saa nne, Bwana akipenda, utangulizi utaanza. Ibada ya kuhubiri itaanza karibu na huu, kama—kama saa nne, nadhani. Nanyi muwe hapa mapema, saa tatu, kuchukua

kadi zenu za maombi. Nao hao wavulana watakuwa hapa wakisambaza kadi za maombi saa tatu, asubuhi ya leo. Vema.

165 Sasa kimbieni nyumbani. Ikiwa inakubidi kula, endelea. Endapo huli, rudi bila kifungua kinywa. Jamani, tunakula kupita kiasi, kwa vyovyote vile. Kwa hivyo basi rudini, mkifunga, mkishangilia, acha moyo wako uwe sawa.

166 Wekeni hilo tu niani mwenu, "Najua Mkombozi wangu yu hai. Ninajua Yeye yu hai. Kengele za furaha zikilia moyoni mwangu! Kwa sababu Yeye alifufuka, nami nitafufuka pia. Kwa maana, tayari nimefufuka, kwa muda, nimeinuliwa pamoja Naye sasa, 'nimeketi mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu.'"

167 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, kila mahali jengoni. Nami nimemwuliza Ndugu Beeler, mmoja wa wachungaji hapa . . .

168 Ndugu Tom Meredith, nilimwona huko nyuma, pia, tutamtumia katika ibada baadaye kidogo.

169 Na sasa, Ndugu Beeler, kama atasonga mbele huku kila mtu akiwa ameinamisha vichwa vyao katika maombi, tutamwomba aturuhusu tuondoke kwa maombi. Vema, Ndugu Beeler, tafadhali.

55-0410S Mkombozi Wangu Yu Hai
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org